Advocates for Basic Legal Equality, Inc.

Legal Aid of Western Ohio, Inc.®

TOGETHER, WE DO THE COMMUNITY JUSTICE

Haki Zako ikiwa Kiingereza Si Lugha Yako ya Msingi:

Shule ya Mtoto Wako na COVID-19

Majengo ya shule yamefungwa kwa kipindi kilichobaki cha mwaka wa shule kutokana na COVID-19. Huenda unawaza kitu ambacho unapaswa kutarajia kutoka kwa shule ya mtoto wako cha kumsaidia mtoto wako kuendelea kujifunza Kiingereza na kufanya kazi ya shuleni.

- Watoto ambao wako na ujuzi mdogo wa Kiingereza wana haki.
- Haki ya kujiandikisha katika shule ya umma iliyoko karibu.
- Haki ya kujifunza Kiingereza.
- Haki ya kushiriki katika masomo na rika zao, huku wakipatiwa usaidizi wa ziada au kubadilishiwa mafunzo ili waweze kujifunza.
- Wazazi ambao wako na ujuzi mdogo wa Kiingereza pia wana haki ya kuwasiliana na shule kwa lugha ambayo wanaweza kuelewa.
- Haki hizi za wazazi na watoto bado zinændelea kutumika hata wakati ambapo majengo ya shule yamefungwa katika mwaka huu wa shule.

Waalimu na shule za mtoto wako lazima washirikiane nawe na mtoto wako na kuwasiliana kwa lugha ambayo unaweza kuelewa. Mawasiliano kati yako na wilaya ya shule na waalimu wako huenda yakawa tofauti. Huenda yakatendeka kupitia simu, ujumbe fupi, programu kama vile TalkingPoints, mikutano kupitia video, madarasa ya mitandaoni, au teknolojia nyingine.

Yafuatayo ni baadhi ya mifano ya habari ambazo shule inapaswa kutoa kwa lugha yako ya msingi.

- Habari kuhusu kufungwa au kufunguliwa tena kwa majengo ya shule
- Jinsi ambavyo shule inaandaa kazi za shuleni kwa mtoto wako (mtandaoni/furushi la makaratasi/simu/n.k.)
- Msaada kwa mtoto wako ili ælewe mælekezo ya kazi ya shuleni
- Alama na Ripoti za matokeo
- Habari kuhusu mpango wa Anayejifunza Kiingereza wa mtoto wako
- Ikiwa shule inaandaa kiamsha kinywa au chakula cha mchana, jinsi ya kupata vyakula hivyo
- Tahadhari za Afya za COVID-19

naAdvocates for Basic Legal Equality, Inc. (ABLE) na Legal Aid of Western Ohio, Inc. (LAWO) ni mashirika ya kisheria yasiyo ya faida yanayoshughulikia mahitaji ya kisheria ya kiraia ya watu binafsi na familia zilizo na mapato madogo katika magharibi mwa Ohio. Habari hizi si ushauri wa kisheria. Ni habari za kawaida. Habari hizi hazitumiki kama mbadala wa kuzungumza na wakili kuhusu hali yako. Bado huenda ukahitaji usaidizi kutoka kwa wakili. Habari hizi ndizo za sasa mnamo Mei 20, 2020, na unapaswa kufahamu kwamba habari kuhusu sheria mpya na ufafanuzi wake huendelea kubadilika.

Zifuatazo ni baadhi ya njia ambazo unaweza kuzungumza juu ya msaada wa elimu ya mtoto wako katika wakati huu ambapo majengo ya shule yamefungwa.

- Muombe mwalimu au shule ya mtoto wako imwite mkalimani wakati ambapo umepiga simu. Shule lazima zipeane wakalimani waliohitimu.
- Waambie waalimu wa ESL/ESOL na waalimu wengine wa madarasani wa mtoto wako iwapo unapenda simu au ujumbe mfupi au programu ambazo huwa unatumia.
- Omba taarifa za mawasiliano za mwalimu (namba ya simu/anwani ya barua pepe/namba ya ujumbe mfupi/programu) ili mtoto wako aweze kuomba usaidizi.
- Uliza jinsi ambavyo Wilaya ya shule inapanga kumsaidia mtoto wako ili ændelee kujifunza Kiingereza.
- Omba mafunzo kupitia video ikiwa uko na simu maizi au kompyuta.
- Uliza ikiwa shule inaweza kuwasaidia kupata intaneti ikiwa hamna intaneti.
- Uliza ikiwa shule inaweza kuwapatia kompyuta au kifaa ikiwa mtoto wako hana.
- Mpigie simu Mratibu wa Wasomi Wa Kiingereza wa shule yako ya Wilaya au Mratibu wa ESL ikiwa waalimu hawawasiliani na wewe. Kwa kawaida, unaweza kupata taarifa zao za mawasiliano kwenye tovuti ya shule.
- Pigia Kituo cha Usaidizi cha Lau cha Idara ya Elimu ya Ohio cha Wanaojifunza Kiingereza, 614-466-4109, ikiwa huwezi kumpata Mratibu wa Anayejifunza Kiingereza wa shule yako ya Wilaya au Mratibu wa ESL.
- Uliza jinsi ambavyo unaweza kupata vyakula vya mtoto wako ikiwa shule inapatiana vyakula na saa au mæneo hayafai kwa familia yako.

Ikiwa una mashaka kuhusu elimu ya mtoto wako au kupata habari kwa lugha yako ya msingi kutoka kwa shule katika au baada ya kipindi hiki cha kufungwa kwa shule kutokana na COVID-19 , wasiliana kupitia Namba ya Legal Aid ili kuomba usaidizi wa kisheria wa bila malipo:

PIGA SIMU

BILA MALIPO

(888) 534-1432

NAMBA YA LEGAL AID

WASILISHA OMBI MTANDAONI
www.LegalAidLine.org

Advocates for Basic Legal Equality, Inc.

Legal Aid of Western Ohio, Inc.®

naAdvocates for Basic Legal Equality, Inc. (ABLE) na Legal Aid of Western Ohio, Inc. (LAWO) ni mashirika ya kisheria yasiyo ya faida yanayoshughulikia mahitaji ya kisheria ya kiraia ya watu binafsi na familia zilizo na mapato madogo katika magharibi mwa Ohio. Habari hizi si ushauri wa kisheria. Ni habari za kawaida. Habari hizi hazitumiki kama mbadala wa kuzungumza na wakili kuhusu hali yako. Bado huenda ukahitaji usaidizi kutoka kwa wakili. Habari hizi ndizo za sasa mnamo Mei 20, 2020, na unapaswa kufahamu kwamba habari kuhusu sheria mpya na ufafanuzi wake huendelea kubadilika.